Mwongozo Wa Mwalimu

8

# Utiifu kwa Mungu

## Kujifunza Kunyenyekea kwa Mwongozo wa Mungu



MVMM

Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

# Utiifu kwa Mungu

## Kujifunza Kunyenyekea kwa Mwongozo wa Mungu

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwalimu

Toleo la Tano

Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

# Utiifu kwa Mungu

## Kujifunza Kunyenyekea kwa Mwongozo wa Mungu

Kimeandikwa Na David Batty
Mwongozo Wa Mwanafunzi
Toleo la tano

Maandiko yanayotumiwa katika kitabu hiki yametoka kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2024, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii yaKiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwenye mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo: *Obedience to God, 5th edition.*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, mashuleni, katika huduma gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vile vile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, kitabu cha kuongoza mafunzo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.org na
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 01-2024

# Utiifu kwa Mungu

Kujifunza jinsi ya kumpenda na kumtii Mungu huwa rahisi kwa watu wengine kuliko wengine. Ni vigumu kwa wengi wetu kumpenda mtu wasiye mwona. Kujifunza jinsi ya kumsikiliza Mungu na kujua wakati Anapokuambia ufanye kitu ni jambo muhimu ambalo Wakristo wapya wanapaswa kujifunza haraka. Lengo kuu la kozi hii ni kutafuta njia tunazoweza kutumia kuonyesha utiifu wetu kwa Mungu.

**1**

### Sura ya 1. Upendo na utiifu

Ni pamoja na kujifunza ni kwa nini Wakristo wanapaswa kumtii Mungu. Pia tutaangazia kwa kina sheria kuu za Mungu.

**2**

### Sura ya 2. Mitazamo na utiifu

Tutajadili athari ya mitazamo yetu kwa tabia zetu. Tutaangazia kwa makini kukuza mitazamo ya utiifu.

**3**

### Sura ya 3. Ni sheria zipi nina paswa kutii?

Sehemu hii inahusika na wajibu wa Mkristo kwa sheria za Mungu kwenye Biblia. Tutajadili jinsi mtu anavyoweza kujua kanuni msingi za kila sheria ya Mungu na kutumia kanuni hizo katika maisha yake ya kila siku. Sehemu hii pia inajumuisha kujifunza kuhusu mapenzi ya Mungu kwa Wakristo.

**4**

### Sura ya 4. Matokeo ya kumtii Mungu

Kile kinachoonekana kuwa kigumu mwanzoni — kumtii Mungu — huleta matokeo mazuri. Tunachunguza mifano kutoka kwa Biblia na pia maisha ya leo ili kuona matokeo ya kumtii Mungu.

**5**

### Sura ya 5. Matokeo ya kutomtii Mungu

Tunajadili athari za kutomtii Mungu, tukichunguza matokeo ya kawaida, nidhamu, adhabu, na kulipiza kisasi kwani zinahusiana na kutotii. Tunangalia pia mambo tunayoweza kujifunza kutokana na kutotii kwa wengine.

## Yaliyomo Katika Mwongozo Huu Wa Mwalimu

Kitabu hiki kina sehemu nne. Kila sehemu imeanza kwa ukurasa wenye rangi ya njano, ambao ni ukurasa ulio na jina la mada.

1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo
2. Mwongozo Wa Mwanafunzi
3. Mwongozo Wa Somo
4. Mtihani Wa Mwanafunzi Na Cheti Cha Somo

Maelezo ya jinsi ya kutumia kila sehemu yanapatikana mara tu baada ya utangulizi wa ukurasa unaofuata.

# Utangulizi

Hili ni somo moja katika mfululizo wa masomo ulioandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha Wakristo wapya. Tunaamini kwamba lipo hitaji kubwa sana siku hizi la kuwasaidia Wakristo wapya ili wahusishe mafundisho ya Kristo na maisha yao ya kila siku kwa vitendo. Mafundisho haya pia yanaweza kutumiwa vizuri sana kwa ajili ya huduma kwa vijana kanisani na watu wazima wanaotamani kufanya Ukristo kuwa sehemu ya maisha yao kila siku.

Kusudi kubwa la somo hili na mfululizo mzima wa *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* ni kuwatambulisha Wakristo wapya kwa maswali muhimu yanayohusu maisha. Hatujaribu kuwapa mafundisho yatakayokuwa ndiyo mwisho kuhusu mada husika.

Kamati ya Mtaala ya Huduma ya Teen Challenge Marekani, ina mpango wa kuendelea kupitia upya na kufanya marekebisho kwa masomo haya. Tunakaribisha mawazo yoyote au hoja za kutusaidia kuyaboresha.

## Jinsi ya kutumia Mwongozo huu Wa Mwalimu

### 1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo

Kurasa za kwanza katika sehemu hii zinatoa mtazamo wa somo zima kwa ufupi.

Ukurasa unaofuata utakuwa ni nakala ya ***Orodha Ya Kazi Za Darasani***. Hii orodha inaonyesha wakati ambapo kila zoezi katika Mwongozo wa Somo linatakiwa kukamilishwa, na wakati kila chemsha bongo na mtihani zitatolewa. Kila mwanafunzi anapaswa kupewa habari stahiki kwa ajili ya ukurasa huo mwanzoni mwa kila somo. Kitabu hiki cha Mwongozo wa Somo tayari kina nakala isiyoandikwa chochote ya fomu hiyo, kwenye jalada la nyuma upande wa ndani.

Kitakachofuata ni mipango kwa ajili ya kufundishia kila somo. Hiyo yote ina kitu kinachoitwa Kweli Kuu ya Kibiblia pamoja na Mstari Mkuu. Hivyo vitu viwili vinaweza kutolewa mwanzoni mwa kipindi cha darasa. Pia vinasaidia kufanya mjadala ulenge yanayotakiwa kwa wakati wote.

Chini ya Kweli Kuu ya Kibiblia na Mstari Mkuu, kuna maelezo machache jinsi ya kufundisha somo lenyewe. Mara nyingi, marejeo yanaelekezwa kwa Mwongozo wa Mwanafunzi au kwa Zoezi linalopatikana katika Mwongozo wa Somo.

Kila somo humalizika kwa shughuli ya kufanya katika “Kufanyia Kazi Somo Maishani.” Umuhimu wa kipengele hiki haueleweki. Wakristo wapya wanahitaji mwongozo ulio wazi kuhusu jinsi ya kuanza kufanyia kazi mafundisho haya katika maisha yao ya kila siku. Hakikisha kwamba una toa nafasi ya kutosha ili kuwasaidia wanafunzi wako kuanzisha shughuli hii.

Mwisho wa kila mpango wa kufundishia somo kuna orodha ya kazi za wanafunzi kufanya.

Mengi katika masomo haya yalikusudiwa kuwa na vipindi vitano vya darasa, kila kimoja kikidumu kwa saa moja. Kipindi cha mwisho darasani ni kwa ajili ya mtihani. Masomo yote 14 katika mfululizo huu yanaweza kukamilishwa katika kipindi cha miezi kati ya mitatu hadi

minne, kama darasa litakutana kwa siku tano katika wiki. Ikiwa unafanya darasa kwa saa moja tu kwa juma, unaweza kukamilisha somo moja kwa mwezi – na mfululizo wote kwa kama mwaka mmoja. Mengi katika haya masomo yanaweza kupanuliwa na kufundishwa kwa muda mrefu, au kwa madarasa zaidi.

## 2. Mwongozo Wa Mwanafunzi

Kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwanafunzi chaweza kutimiza makusudi mawili. Unaweza kutaka wanafunzi wasome kurasa husika katika kujiandaa kwa ajili ya somo linalofuata. Au, unaweza kuwataka wakisome baada ya wewe kufundisha somo, ili kufanya kama marudio na kuwa kama njia ya kusisitiza na kukazia kilichofundishwa darasani.

Tunakutia moyo uwaambie wanafunzi wajiandikie notsi darasani, hata ingawa utawapa Mwongozo Wa Mwanafunzi. Wanayojiandikia wenyewe pamoja na mazungumzo na mijadala darasani vitawasaidia sana kuelewa vizuri baadhi ya mada zinazoshughulikiwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

## 3. Mwongozo Wa Somo

Mazoezi yaliyo katika Mwongozo wa Somo yameandaliwa ili kumpa mwanafunzi kazi ya kufanya nje ya darasa. Baadhi ya kazi-mradi hizo zinasaidia kumwandaa mwanafunzi kwa ajili ya somo la darasa linalofuata.

Mengi ya mazoezi haya yamekusudiwa kuwasaidia wanafunzi wajikite ndani zaidi na kutazama baadhi ya maswala yanayojadiliwa darasani kwa kina. Lengo kuu la kazi hizo nyingi ni kuwaasaidia wanafunzi wagundue njia za kufanyia kazi hizo za kweli za Biblia katika maisha yao ya kila siku.

## 4. Mtihani Wa Mwanafunzi na Funguo la Majibu ya Mtihani

Mitihani hii imeandaliwa ili kutoa kipimo rahisi tu cha maendeleo ambayo kila mwanafunzi alipata katika uelewa wa kweli za Biblia zinazoshughulikiwa katika somo hili. Karatasi ya Majibu kwa ajili ya mtihani husika iko mara tu baada ya ukurasa wa mwisho wa ile nakala mfano ya mtihani wa mwanafunzi, katika Mwongozo huu wa Mwalimu.

## 5. Cheti Cha Somo

Cheti cha somo ni kwa ajili ya kuwatambua wale wanaomaliza kazi yote inayotakiwa kwa ajili ya somo hili na kufaulu mtihani. Mfano wa cheti hicho cha somo upo katika ukurasa wa mwisho wa kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwalimu. Cheti cha Kufuzu pia kinapatikana kwa wale wanafunzi wanaomaliza masomo yote 14 katika mfululizo huu wa *Mafunzo ya Vikundi Ya Maisha Mapya*. Pia, mfano upo katika kile kitabu kinachoitwa ***Kuwatambulisha waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya***.

# Jinsi Masomo Haya Yalivyotokea

Sulemani alisema, hakuna kitu kipya chini ya jua. Maneno hayo yanaweza kufaa hata kuhusu masomo haya. Mawazo yake mengi si mapya. Tunataka kutoa shukrani zetu maalum kwa Institute in Life Principles (Taasisi Ya Kanuni Za Maisha) kwa ushawishi mkubwa katika maisha ya watu waliotayarisha masomo haya. Masomo mengi yana alama za huduma hiyo ya Institue in Life Principles.

Nataka pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengi sana na maelfu ya Wakristo wapya ambao wametumia masomo haya katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita. Mawazo yao yamekuwa na mchango mkubwa sana katika maandalizi ya masomo haya.
Pia ninamshukuru sana Ndugu Don Wilkerson kwa kunipa nafasi ya kufanya kazi katika kituo cha huduma ya Teen Challenge pale Brooklyn, New York, tokea mwaka wa 1971 hadi 1975. Katika miaka hiyo ndipo matayarisho yalipoanza ya masomo haya yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya*.

Toleo la tano la *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* lilitayarishwa kwa msaada wa kamati ya Mitaala ya huduma ya Teen Challenge Marekani. Natoa shukrani maalum kwa wote waliosaidia katika mapitio na marekebisho hayo.

# Sera Kuhusu Kunakili Machapisho Haya

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi kinachohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* kinalindwa na Sheria za Haki Miliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali fulani, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kwenye mtandao kwa tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Dave Batty

# Pendekezo Kuhusu Mpangilio Wa Kufundisha

Somo hili ni moja kati ya 14 katika mfululizo wa *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya*. Masomo yote 14 yameorodheshwa hapa kama pendekezo la jinsi ya kuyafundisha. Mfuatano huu ulitayarishwa kwa ajili ya ufundishaji endelevu wa masomo haya. Tunaweza kuutazama kama picha ya gudurumu lenye vyuma kumi na vinne. Masomo haya hayategemei linalotangulia. Kila somo linasimama lenyewe. Basi, mwanafunzi anaweza kujiunga na madarasa wakati wowote na akaingia tu vizuri kwenye mfumo.

1. Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?
2. Kuitazama Biblia Kwa Haraka
3. Mtazamo
4. Majaribu
5. Maisha Ya Kikristo Yenye Mafanikio (ni pamoja na mafunzo juu ya huduma ya Roho Mtakatifu.)
6. Kukua kupitia kufeli
7. Matendo Ya Kikristo (Mahusiano Katika Kanisa La Mahali)
8. Utiifu kwa Mungu
9. Utiifu kwa Mwanadamu
10. Hasira na Haki za Kibinafsi
11. Jinsi Ya Kujifunza Biblia
12. Kujipenda na Kujikubali Mwenyewe
13. Mahusiano yako wewe Binafsi na Wengine
14. Nguvu Ya Kiroho na Mambo Yasio Ya Kawaida

Tazama kitabu kiitwacho, ***Kuwatanguliza waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya***, ili kupata maelezo zaidi juu ya kufundisha masomo hayo.

# Mipangilio ya Masomo

# Kwa Mwalimu

Angalia ukurasa wa 4 wa Mwongozo wa Mwalimu kwa habari zaidi
kuhusu matumizi ya mipangilio hii ya masomo

# Maelezo ya jumla ya kozi

**1.** Unaweza kutanguliza kozi hii kwa wanafunzi siku moja au mbili kabla ya kipindi cha kwanza darasani na kuwapa kazi zao za kwanza. Zoezi la kwanza katika Mwongozo wa somo linahitaji kukamilishwa kabla ya kipindi cha kwanza darasani. Wape Wanafunzi Mwongozo wao na uwaulize wasome Sura ya Kwanza, ambayo itajadiliwa katika kipindi cha kwanza darasani.

**2.** Kwenye ukurasa unaofuata katika mwongozo huu wa mwalimu, kuna nakala ya *Orodha ya kazi Darasani* inayotoa tarehe ambayo kila kazi inapaswa kukamilishwa. Waagize wajaze tarehe zinazofaa katika nakala tupu kwenye *Orodha ya kazi Darasani* iliyo nyuma ya Mwongozo wao wa somo.

**3.** Kila mpangilio wa somo una "Zoezi la utangulizi wa somo" zaidi ya moja vitakavyotumika mwanzoni mwa somo hilo. Kusudi kuu la kufanya haya ni kuwasaidia wanafunzi kuwa makini katika mada kuu ya somo hilo. Tunataka kuunda mazingira mazuri na yenye uwazi yatakayowafanya wanafunzi wote kuhisi huru kushiriki katika majadiliano darasani.

**4.** Kozi hii inahusiana kwa karibu na *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* kwenye kozi ya *Utiifu kwa Mwanadamu*. Unapofundisha kozi hii, hakikisha kuwa haujatumia muda mrefu katika sehemu ya kuwatii viongozi wetu kwa kuwa sehemu hii itajadiliwa katika kozi nyingine. Kwa kweli kuna mwingiliano wa maswala na kanuni za kibiblia katika suala la kumtii Mungu na kuwatii viongozi wetu.

**5.** Kama ratiba yako inaruhusu vipindi zaidi ya 5 vya darasa vya kufundisha kozi hii, unaweza kugawa somo la 3 (sura ya 3 katika Mwongozo wa Mwanafunzi) na kuongeza kipindi cha ziada cha darasa unapoangazia mada ya, **"Mapenzi ya Mungu" ni nini?** Tazama ukurasa wa 26-28 katika Mwongozo wa Mwanafunzi. Mpangilio wa somo kwa mwalimu #3, hoja14 na 15 zinashughulikia maswala haya kwenye ukurasa wa 31-32 katika Mwongozo huu wa Mwalimu.

# Orodha ya kazi za Darasani

**Mada ya Somo:** Utiifu kwa Mungu

**Chemsha Bongo** Mstari wa kumbukumbu — Tarehe

1. Marko 12:30 — Siku ya 2
2. Yohana 13:34-35 — Siku ya 3
3. ______

**Zoezi** Tarehe ya Kuwasilisha

1. Siku 1
2. Siku 2
3. Siku 4
4. Siku 3 au 4

**Mtihani** Tarehe Siku 5

# 1 Somo la 1
# Upendo na utiifu

## 1. Kweli kuu ya Kibiblia

Njia bora ya kumtii Mungu ni kuonyesha upendo wangu kwa Mungu kwa njia zenye maana katika maisha yangu ya kila siku.

## 2. Mstari mkuu: Marko 12:30 Biblia Takatifu (SUV)

Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote.

## 3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili

Sura ya 1 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi inaendana na somo hili. Zoezi la 1 *"Ushauri wa Biblia Kuhusu Kumtii Mungu,"* litatumika katika somo hili.

## 4. Zoezi la utangulizi wa somo (dakika 5)

Tumia mojawapo ya visisimuzi vifuatavyo kuwasaidia wanafunzi kuwa makini darasani kwa mada ya leo—kumtii Mungu.

A. **"Makubaliano niliyoweka na Mungu."** Waulize wanafunzi ikiwa wamewahi kuwa na makubaliano na Mungu. Pengine walikuwa katika hali ngumu na wakasema, "Mungu, ikiwa utaniondoa katika hali hii ngumu, Nitakutumikia maishani mwangu." Unaweza kutoa mfano mmoja au miwili ya "makubaliano" waliyokubaliana na Mungu. Wape wanafunzi pia nafasi ya kusimulia kuhusu makubaliano waliyokubaliana na Mungu.

B. **Toa mfano kutoka kwa maisha yako (au maisha ya Mkristo mwingine) wa wakati ambao Mungu alikuambia ufanye jambo fulani.** Kwa mtazamo wako wakati huo lilionekana kama jambo baya kufanya, hata hivyo uliamua kumtii Mungu. Na matokeo yakawa mazuri zaidi kuliko ulivyotarajia. Mungu alikuonyesha kuwa kumtii ndiyo njia bora.

C. Igiza mchezo wa **"Let's Trade Your Salvation,"** (Natufanyie biashara wokuvu wako) kutoka kwa rekodi, "Fun In the Son,," na Isaac Air Freight (1978, Maranatha Music, Costa Mesa, CA). Mchezo huu wa kuchekesha umeandaliwa kutokana na vipindi vya Runinga. Mkristo anapewa nafasi ya kuuza wokovu wake kwa zawadi mbalimbali.

**5. Kubadilisha uhusiano na Mungu**
**(dakika 2-3) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 4**

Ikiwa darasa lako lina Wakristo wapya, basi kuna uwezekano kuwa kumekuwa na mabadiliko makubwa katika uhusiano wao na Mungu kwa siku za hivi karibuni. Uhusiano huu mpya wao na Mungu unatoa msingi wa njia mpya ya kuishi. (Rejelea ukurasa wa 4 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.)

Walipokuwa Wakristo, walimwomba Mungu awe Kiongozi wa maisha yao. Tazama Wakolosai 1:21-22. Katika kitabu cha Yohana 1:12 na Wagalatia 3:26 Mkristo anaelezewa kama mwana wa Mungu. Mungu anachukua jukumu la kuwa Kiongozi wao, Baba yao. Anampa Mkristo mpya jukumu la kumtii.

Kwa hivyo unapojifunza mada hii ya kumtii Mungu, wahimize wanafunzi kujiuliza maswali haya:

Inamaanishaje kuwa mwana wa Mungu?

Tunawezaje kukuza uhusiano wetu na mtu ambaye hatumwoni?

Je, nina uhusiano wa aina gani na Mungu?

**6. Jadili Hoja A-1, "Je, ni mahusiano gani unayothamini zaidi leo?"**
**(Dakika 2-3) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 4-5**

Hoja A, "Hitaji la Mahusiano mapya," ina vidokezo 3. Hoja hizi zitasaidia kuweka msingi wa somo hili la kwanza. Uwe mwangalifu usiingilie maswala haya kwa undani. Hoja B-E inahitaji muda zaidi katika somo la leo.

Sisitiza umuhimu wa kila mtu kuchukua muda kujibu swali #1 - "Je, ni mahusiano gani unayothamini zaidi hii leo?"

Katika dunia ya leo. vijana wengi wanalelewa katika utamaduni uliojaa jumbe mbalimbali kuhusu mahusiano. Jumbe ambazo zinaenda kinyume na Biblia. Mtazamo mwingine ni kwamba wengi wametoka katika familia zilizovunjika na hivyo uhusiano mzuri si sehemu ya maisha yao.

Msingi wa kozi hii ni kwamba kila mmoja anapaswa kuthamani pakubwa hitaji la kuwa uhusiano wa kibinafsi na Yesu Kristo. Hii ni zaidi ya kuomba sala rahisi ya kuokolewa kutoka kwa dhambi.

**7. Jadili Hoja A-2, "Je, tunakuzaje mahusiano mapya?"**
**(Dakika 2-3) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5**

Fanya majadiliano haya yawe mafupi.

Sisitiza umuhimu wa kuvunja uhusiano na watu ambao huturudisha katika maisha yetu ya kale ya dhambi.

Lazima wachague kuwa na uhusiano mpya kwa kuwa wamefanya uamuzi wa kuwa Wakristo. Waambie wazungumzie wanayoyajua kuhusu suala hili la kuwa na uhusiano mpya baada ya kuwa Mkristo.

Uliza swali hili**, "Je, unawezaje kuwa na uhusiano wa ndani zaidi na Mungu?"** Fanya majadiliano haya yawe mafupi. Baada ya kutoa baadhi ya majibu, waelekeze kwa hoja zilizoorodheshwa kwenye ukurasa wa 5 katika Mwongozo wa Mwanafunzi. Eleza kuwa kwa sehemu iliyosalia ya kozi hii, tutaangazia zaidi njia moja ya kukuza uhusiano wa ndani zaidi na Mungu – njia hiyo ni "kumtii Mungu."

Mambo mengine yaliyoorodheshwa pia ni muhimu sana, lakini yatashughulikiwa wakati mwingine, katika kozi tofauti ambayo si ***Utiifu kwa Mungu***.

**8. Jadili Hoja A-3, "Mungu anataka kuwa Baba yako."**
**(Dakika 5-7) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5-7**

Anza majadiliano yako hapa kwa kuwaambia wanafunzi wako wasome 2 Wakorintho 6:18. Onyesha uhusiano ambao Mungu anataka. Hatuiti wateja Wake, wala watumwa Wake. Anataka tuwe wana Wake.

> **2 Wakorintho 6:18 Biblia Takatifu (SUV)**
>
> **Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi.**

Jadili tatizo ambalo wengine wanalo kuhusu "dhana ya baba," kama ilivyoelezewa kwenye ukurasa wa 5-6 wa Mwongozo wa Mwanafunzi. Waambie wanafunzi wako wazungumze kuhusu baba yao, na anavyofanana au kutofautiana na Jessie na Eric.

Hapa hatujaribu kusuluhisha maswala yote ya zamani, tunaonyesha kuwa ikiwa wanafunzi wako wamekuwa na matatizo katika familia zao, wanaweza kupata tatizo kubwa zaidi la kukabili tatizo hili. Hata hivyo, Mungu anataka uhusiano mzuri wa kibinafsi na wa karibu nao. Anataka kuwa baba yao ambaye hawakuwahi kuwa naye.

Unaweza kurejelea orodha ya baadhi ya njia za kuonyesha uhusiano wa kibinafsi na Mungu katika ukurasa wa 6-7 katika Mwongozo wa Mwanafunzi. Unaweza kukosa wakati wa kusoma na kujadili kila moja kwa undani, lakini wahimize kuyasoma wenyewe kwa undani zaidi kwa wakati wao.

**9. Jadili Hoja B. Je, utii una nafasi gani katika uhusiano wangu na Mungu?**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi. ukurasa wa 7-8**

Fanya majadiliano haya yawe mafupi.

Waulize wanafunzi wako, **"Kutii sheria za Mungu kuna nafasi gani katika uhusiano mzuri na Mungu?"**

Baada ya wanafunzi kujibu, sema kuwa mipaka ni njia ya Mungu ya kutulinda. Haitunyimi uhuru, inatulinda ili tuweze kufurahia uhuru wa kweli katika maisha yetu ya kila siku.

Usijadili kwa kina hoja ndogo 1, Elekeza mjadala wako kwa hoja 2, *"Sheria kuu ya Mungu."* Waambie wanafunzi wako wasome Mathayo 22:35-40.

Sema kuwa sheria mbili kuu za Mungu ni za upendo—pia zote mbili zinahusiana na mahusiano. Waelekeza kwa Mathayo 22:40 – kwamba sheria zingine zote kwenye Biblia zinategemea sheria hizi mbili.

**10. Jadili Hoja C. “Kwa nini umtii Mungu?”**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 8-9**

Fanya majadiliano haya yawe mafupi.

Sisitiza hoja iliyozungumziwa katika aya 2 za kwanza kwenye sehemu hii katika ukurasa wa 8 katika Mwongozo wa Mwanafunzi. Utiifu na upendo zina uhusiano wa karibu sana.

Waambie wanafunzi wako wasome Yohana 14:15 na wajadili uhusiano kati ya upendo na kutii sheria za Mungu. Sema kuwa kila wakati tunapotii mojawapo ya sheria za Mungu, matendo yetu humwambia Mungu, “Nakupenda”.

**11. Jadili Hoja D-1. “Ninaweza kuanza vipi kumpenda Mungu?”**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 9-10**

Waambie wanafunzi waeleze jinsi wanavyojifunza kuonyesha upendo wao kwa Mungu. Ikiwa wanakawia kujibu, waambie wasome 1 Wakorintho 13 ili kuona mambo wanayoweza kufanya kuonyesha upendo wao kwa Mungu.

Eleza kuwa kumpenda Mungu sio tu kwa mambo tunayomfanyia Mungu moja kwa moja, mbali ni kwa jinsi tunavyowatendea watu wengine.

Waambie wanafunzi wajibu swali la 2 na la 3 kwenye Zoezi 1 kutoka kwa Mwongozo wa Somo.

**Swali 2: Ni vipi Yakobo anaeleza kupitia Kwa sheria za Mungu katika Yakobo 1:25?**

**Swali 3: Ni nini Yakobo anasema ni lazima nifanye iwapo ningetaka kutii sheria za Mungu? (Yakobo 1:25) Andika mambo 2.**

**12. Jadili Hoja D-2. “Je, itakuwaje ikiwa sina nguvu ya kumtii Mungu?”**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 10-11**

Wape wanafunzi wako nafasi ya kusoma na kujadili maandiko haya mawili 2 Timotheo 1:7 na 2 Wakorintho 12:9 ambayo yanazungumzia moja kwa moja suala hili. Eleza kwamba tunaweza kuwa na nguvu kila siku tunaposimama katika ahadi za Mungu - pamoja na mistari hii.

Sisitiza umuhimu wa <u>kutaka</u> kutii sheria za Mungu.

**13. Jadili Hoja D-3. “Na je, iwapo sihisi upendo wowote kwa Mungu?”**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 11**

Anza kwa kujadili jinsi utamaduni wetu wa kisasa unavyoeleza upendo-mara nyingi huangazia “hisia” ya mapenzi.

Hata hivyo upendo wa kweli ni zaidi ya hisia-ni kujitolea kwa moyo. Ni kujitolea kumtendea mtu mwingine mambo yanayoonyesha upendo-kwa maneno yetu, mitazamo yetu, matendo yetu, na mawazo yetu.

1

Eleza kuwa sheria kuu katika Biblia haituamuru tuwe na hisia fulani kwa Mungu.

Wape baadhi ya wanafunzi fursa ya kueleza jinsi hisia zao kwa Mungu zilivyobadilika walipokuwa Wakristo. Je, walimwona Mungu kwa njia ya kipekee? Je, mioyo yao ilibubujikwa na upendo? Au ilikuwa kinyume kabisa? Je, hawakuhisi chochote?

Eleza kuwa mambo yote haya mawili ni ya kawaida-hisia za upendo mkuu kwa Mungu, au kutokuwa na hisia zozote maalum kwa Mungu-hakuna aliyekosea.

Tunapokua katika uhusiano na Mungu, tutaanza kuhisi upendo zaidi kwa Mungu wakati matendo na mawazo yetu yanalenga kumpenda na kumtii Mungu.

Wengi ambao wana hisia maalum za upendo kwa Mungu wanaweza kuamka siku moja na kukosa hisia hizo. Haimaanishi kwamba Mungu amewaacha. Haimaanishi kwamba hawampendi Mungu tena. Hisia huja na kwenda-hiyo ni hali ya kawaida. Ikiwa tunahisi upendo au la, tunapaswa kuendelea kuwa na mienendo ya utiifu kwa Mungu na kwa sheria Zake.

**14. Jadili Hoja E. Je, nia za mtu huwa na nafasi gani katika kumtii Mungu? (Dakika 5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 11-13**

Jadili hoja hii kwa kifupi kama jambo la mwisho katika somo hili. Pengine hautakuwa na wakati wa kutosha wa kujadili suala hili kwa kina.

Kwanza, hakikisha kuwa wanafunzi wako wameelewa maana ya neno, “nia.”

Eleza kuwa nia ni suala la kibinafsi kati yako na Mungu. Hatuwezi kutazama ndani ya moyo wako na kuona nia zako ni gani. Kwa hivyo hili ni suala la kibinafsi. Hata hivyo, Mungu huona nia zetu, kama ilivyoandikwa katika Mithali 21:2 na 20:27.

Sisitiza umuhimu wa upendo kama nia yetu kuu ya kumtii Mungu. Woga ni sababu nyingine—woga wa kwenda kuzimu ikiwa hatutatii. Lakini tunahitaji mengi zaidi ya woga kukuza uhusiano wa karibu wa kibinafsi na Mungu.

Jadili nia zingine za kumtii Mungu, kama vile hatia, wajibu, ujanja.

**15. Matumizi Binafsi (dakika 5-15)**

Angazia matumizi ya kibinafsi hii leo kwa mambo mawili.

A. Wanapaswa kutafuta njia za kuonyesha upendo wao kwa Mungu. Wahimize kutafuta mambo madogo ambayo wanaweza kumfanyia Mungu kama sehemu ya kawaida ya maisha yao ya kila siku. Sisitiza umuhimu wa uthabiti.

B. Wahimize kuchukulia mapenzi kuwa sababu yao kuu ya kumtii Mungu. Wahimize pia kujitolea kabisa kumtii Mungu. Hili linapaswa kupewa kipaumbele maishani mwao.

Kwa matumizi binafsi, kila mwanafunzi aandike sala kwa Mungu, akimshukuru kwa kuwa yeye ni Kiongozi mwenye upendo. Washauri wamwambie kuhusu upendo wao kwake na hamu yao ya kutii sheria Zake. Wahimize kumwambia Mungu kuhusu nia zao za kumtii.

Kisha wapange wanafunzi wawili wawili na kuwaagiza kusoma maombi yao kwa mwenzao.

Waache kwa siku nzima watafute njia za kuonyesha upendo na uttifu wao kwa Mungu. Eleza jinsi Zoezi 1 katika Mwongozo wa somo linavyoingiliana na haya.

**16. Kazi ya ziada.**

A. Ikiwa haujawapa wanafunzi Mwongozo wa wanafunzi, hii ni fursa nzuri ya kuwapa. Waambie wanafunzi wasome sura 2 kutoka kwa Mwongozo wa wanafunzi kabla ya kipindi kifuatacho.

B. Sahihisha kazi ya Zoezi 1 kwenya mwongozo wa somo, *"Ushauri wa Biblia Kuhusu Kumtii Mungu,"* mwishoni mwa darasa

C. Unaweza kuwaambia wanafunzi wako wasome 1 Samweli 15 ili kujiandaa kwa kipindi kijacho cha darasa. Tazama Hoja #7 katika Mpangilio wa Somo, Somo la 2 (Mwongozo Wa Mwalimu - ukurasa 19) kwa habari zaidi.

**17. Tadhmini ya somo**

Orodhesha maoni yako ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu gani ziliokuwa bora zaidi?
Ni sehemu gani zilizokuwa ngumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 2
# Mitazamo na utiifu

2

**1. Kweli Kuu Ya KiBiblia**

Wakristo wanapaswa kuwa na mitazamo ya utiifu itakayotumika wanapomtii sheria Zake Mungu.

**2. Mstari Mkuu:**

Wafilipi 2:5 Biblia Takatifu (SUV)

Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 2 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi unaenda pamoja na somo hili. Zoezi la 2, *"Nia yangu ya kumtii Mungu,"* kutoka kwa Mwongozo wa somo pia litatumika katika somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (dakika 5-10)**

Anza darasa kwa kujadili zoezi la 2 kwenye Mwongozo wa somo, *"Nia yangu ya kumtii Mungu."* Wape wanafunzi wachache nafasi waelezee majibu walioyatumia kwa zoezi hili.

Ikiwa wanafunzi hawataki kusema majibu yao, soma mfano mmoja au miwili kutoka kwa wanafunzi wako wa zamani. Tumia nafasi hii kurejelea na kufafanua jinsi hali yoyote inaweza kuwa njia ya kutii sheria kuu zaidi kwenye Biblia. Jambo la msingi ni kufanya anavyotaka Mungu, na kufanya nia yetu iwe ni upendo.

**5. Nia na mitazamo (dakika 1-2)**

Tumia maraejeleo haya ya kipindi cha darasa la kwanza kuingia katika somo la leo. Taja kuwa nia zako zinahusiana kwa karibu sana na mitazamo yako. Katika kipindi hiki cha darasa, tutajadili nafasi ya mitazamo yetu katika kumtii Mungu. Lengo letu kuu ni kutafuta njia nzuri za kuonyesha mitazamo ya utiifu kwa Mungu.

**6. Ufafanuzi wa mitazamo (dakika 3-5)**

Jadili kwa kifupi "mitazamo" ni nini. Unaweza kukagua yaliyomo katika kozi iitwayo *Mitazamo* kutoka kwa *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya*. Katika sura ya kwanza utapata maelezo ya mitazamo inavyokuzwa. Hakikisha darasa lako linaelewa mitazamo ni nini. Hii ni orodha ya fafanuzi zilizotolewa katika Mwongozo wa Mwanafunzi wa ***Mitazamo*** mwanzoni mwa sura ya kwanza.

**Mtazamo ni nini?**

1. Mfumo wa mafikira
2. Maoni
3. Jinsi unavyofikiria
4. Mazoea ya mafikira
5. Msimamo
6. Mawazo niliojifunza
7. Msimamo wa kiakili kwa kulingana na ukweli au hali
   (Tafsiri ya Webster's saevent New Collegiate Dictionary)

Mara tu wanafunzi wako watakapoelewa wazi maana ya neno mtazamo, onyesha jinsi mitazamo yetu inavyoathiri tabia zetu. Tunafanya yale tunayoyafikiria. Tabia zetu zinaonyesha mitazamo yetu. Ikiwa wanataka kumtii Mungu, basi wanapaswa kuwa na mitazamo ya utiifu.

**7. Jadili Hoja A. Angalia mitazamo inayofanya iwe rahisi kutomtii Mungu. (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwaanafunzi, ukurasa wa 14-15**

Inaweza kuwa rahisi kwa wanafunzi wako kuona mitazamo ya kutotii katika maisha yao ikiwa wataangalia wanavyowajibu viongozi wao. Ikiwa wana mitazamo hii ya kutotii kwa viongozi wao wa kidunia, kuna uwezekano mkubwa kuwa wana mitazamo hiyo hiyo kwa Mungu.

Waambie waangalie orodha ya mitazamo ya kutotii kwenye ukurasa wa 14 wa Mwongozo wa Mwanafunzi. Wahimize kuchagua mitazamo wanayoiona kuwa rahisi kuonyesha katika maisha yao ya kila siku.

Unaweza kujadili kwa kifupi mfano wa tukio kwenye soko la vyakula kama njia moja ya kuwasaidia kuona jinsi mitazamo inaweza kuathiri matendo ya kutotii. Tumia tukio hilo pia kuwasaidia kuona uhusiano kati ya kuwatii watu wengine na kutii sheria za Mungu.

Jadili hadithi ya Mfalme Sauli kutoka 1 Samweli 15. Mistari miwili mikuu (mstari 22-23) imenukuliwa kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi katika ukurasa wa 15, lakini hadithi yote inatoa mfano mzuri na wa kusikitisha wa kutomtii Mungu.

Taja kilichotokea awali katika 1 Samweli 13 pale ambapo Sauli pia hakumtii Mungu.

Mungu anaweka wazi Anachofikiria kuhusu mitazamo ya kutotii katika 1 Samweli 15:22-23. Kutii ni bora kuliko dhabihu yoyote ambayo mtu anaweza kutoa. Mungu huona mtazamo wa kutotii kuwa sawa na dhambi ya uchawi. Mtazamo wa ukaidi ni mbaya na ni sawa na kuabudu sanamu.

2

**8. Jadili Hoja B. “Kuza mitazamo ya utiifu”**
**(dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 15-19**

Tanguliza sehemu inayofuata ya somo inayohusiana na mitazamo ya utiifu. Tumia orodha ya mitazamo ya kutotii na kisha uwaambie wanafunzi wako wafikirie tofauti ya kila moja, au mtazamo wautiifu. Jadili kwa kifupi maana ya kila mmoja. Jaribu kutoa mfano kifupi wa kila moja unapofafanua.

Eleza kuwa Yesu alionyesha kupitia maisha yake kwamba mitazamo hii inaweza kutimizwa. Mitazamo hii ya utiifu ilidhihirika pakubwa maishani Mwake na iliathari pakubwa uumbaji wa utu wake. Kwenye Bustani ya Gethsemane, tunapata picha wazi ya Yesu akionyesha mitazamo ya utiifu. Taja kwamba mitazamo ya utiifu hufanya iwe rahisi kumtii Mungu.

Kurasa 16-19 katika Mwongozo wa Mwanafunzi zinatoa maelezo ya ziada juu ya kila mojawapo ya mitazamo ya utiifu. Ingekuwa vyema kusema kuwa Yesu alifanya kila moja ya mitazamo hii ya utiifu kuwa sehemu ya maisha yake ya kila siku.

Toa muhtasari wa kila moja ya mitazamo 4 ya utiifu. Hakikisha kuwa wanaelewa ufafanuzi wa kila mtazamo. Unaweza kumuliza mwanafunzi mmoja atoe mfano wa jinsi anatumia moja ya mitazamo hii katika maisha yake ya kila siku.

**Mitazamo minne ya utiifu**

1. Mtazamo wa heshima
2. Mtazamo wa mtumishi
3. Mtazamo wa shukrani
4. Mtazamo wa utulivu

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 16-19*

**9. Mitazamo ya ya utiifu ya Ibrahamu (dakika 5-7)**

Hadithi ya Biblia katika kitabu cha Mwanzo 22:1-19 inaonyesha jinsi’ mitazamo ya utiifu ya Ibrahimu ilimwezesha kumtii Mungu wakati Alimwambia afanye jambo gumu. Hii ndio hadithi ya Ibrahimu kumtoa mwanawe Isaka kama kafara kwenye madhabahu.

Jadili ni mitazamo ipi ya utiifu ambayo Ibrahimu alitumia katika hali hii. Waambie wasome Waebrania 11:17-19 ili kupata ufahamu zaidi kuhusu mawazo ya Ibrahimu wakati wa mtihani huu mgumu.

**10. Kuonyesha mitazamo ya utiifu**
**(dakika 5-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 15-19**

Chagua mojawapo ya mitazamo ya utiifu na ujadili kwa kina jinsi inavyoathiri maisha ya Mkristo. Majadiliano yako yaangazie jinsi ya kukuza na kuonyesha mtazamo huu. Pia tenga wakati wa kujadili jinsi mtazamo huu unaathiri uhusiano wako na Mungu. Jaribu kutoa mifano tofauti ya jinsi mtazamo huu unaathiri tabia yako.

Ikiwa unao wakati, fuata muundo huo huo wa majadiliano kwa kila mtazamo wa utiifu.

Hii ni mistari minne inayozungumzia heshima. Maandiko haya yanaweza kutumika katika majadiliano yako ya kuwa na mtazamo wa heshima.

**Wakolosai 3:25 Biblia Takatifu (SUV)**

**Maana adhulumuye atapata mapato ya udhalimu wake, wala hakuna upendeleo.**

**Waefeso 6:9 Biblia Takatifu (SUV)**

**Nanyi, akina bwana, watendeeni wao yayo hayo, mkiacha kuwaogofya, huku mkijua ya kuwa yeye aliye Bwana wao na wenu yuko mbinguni, wala kwake hakuna upendeleo.**

**Warumi 12:10 Biblia Takatifu (SUV)**

**Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu.**

**1 Petro 3:15 Biblia Takatifu (SUV)**

**Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu.”**

Hapa kuna mapendekezo kadhaa ya jinsi mtu anavyoweza kuonyesha mtazamo wa heshima.

1. Niwafanyie wanaofanya kazi chini yangu mema.
2. Usiwe mgumu kwa mtu kuliko vile angelikuwa kwangu ikiwa angekuwa Mungu.
3. Kumbuka kuwa mmiliki wangu ni Mungu.
4. Heshima huwa rahisi ikiwa ninampenda mtu huyo.
5. Heshima inapaswa kuonyeshwa, sio tu kufikiriwa.

**11. Kufanana zaidi na Kristo (dakika 3-5)**

Kwa kutamatisha majadiliano juu ya mitazamo hii 4 ya utiifu, onyesha umuhimu wa usawa. Tunapoendeleza mitazamo hii ya utiifu na kujitahidi kuondoa mitazamo ya kutotii, tutazidi kufanana na Kristo. Tutakaribia kutenda yale mstari mkuu katika somo hili unasema.

Jadili suala la "utiifu wenye hekima" ulioonyeshwa kwenye ukurasa wa 19 wa Mwongozo wa Mwanafunzi. Mitazamo hii ya utiifu pia inamaanisha utiifu wa hekima. Ukweli wa kiroho si utiifu usio na maarifa. Yesu alikuwa mtiifu kwa Mungu na kwa amri Zake. A*lichagua* kufanya hivyo. Maisha yake yanaweza kuonekana kuwa ya utiifu wenye maarifa. Pia, onyesha kuwa mtu mwenye busara anapenda kumtii Mungu na sheria Zake.

**12. Matumizi ya Kibinafsi (dakika 5-10)**

Kwa matumizi ya kibinafsi hii leo, kila mwanafunzi afanye tathmini binafsi ya yake maisha

Waache watathmini mitazamo inayosababisha kutotii. Kwa kutumia orodha iliyopo kwa ukurasa wa 14 katika Mwongozo wa Mwanafunzi, waache waandike kiwango cha kutotii maishani mwao kwa kutumia alama 1-5. "1" inamaanisha mtazamo ni mdogo sana, hakuna shida hata kidogo. "5" inamaanisha mtazamo ni mkubwa sana katika maisha yao.

Kisha waacha watathmini viwango vyao vya utiifu, wakitumia alama zile zile. "1" ikimaanisha mtazamo huo ni dhaifu sana katika maisha yao (na unahitaji kukua sana). "5" ikimaanisha mtazamo mkubwa maishani mwao.

Waambie waandike angalau jambo moja ambalo wanaweza kufanya ili kuimarisha zaidi tabia ya utiifu. Waagize pia waandike jambo moja ambalo wanaweza kufanya ili kuondoa moja ya mitazamo ya kutotii waliyonayo katika maisha yao.

**13. Kazi**

A. Sahihisha Zoezi 2 la Mwongozo wa somo la, *"Nia yangu ya kumtii Mungu,"* mwishoni mwa darasa.

B. Mwishoni mwa darasa, wape mtihani kuhusu Marko 12:30.

C. Waambie wanafunzi wasome Sura ya 3 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi ili kujiandaa kwa kipindi kifuatacho cha darasa

**14. Tathmini ya Somo**

Orodhesha maoni yako ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu gani ziliokuwa bora zaidi?
Ni sehemu gani zilizokuwa ngumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 3
# Nitatii sheria zipi?



**1. Kweli Kuu Ya KiBiblia**

Kutii sheria za Mungu ni jambo la maana ninaloweza kufanya leo.

**2. Mstari Mkuu:**

Yakobo 1:25 BibliaTakatifu (SUV)

Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya kwanza ya mwongozo wa wanafunzi inaendana na somo hili. Zoezi la 4, *"Kuangalia kwa makini sheria moja,"* katika Mwongozo wa somo linaweza kutumika na somo hili, na/au na somo linalofuata.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (dakika 3-5)**

Anza darasa kwa kuuliza maswali haya. Wape wanafunzi nafasi ya kutoa maoni yao na waeleze ni kwa nini wamechukua msimamo huo.

(1) Je, Wakristo wanapaswa kutii sheria zote za Mungu zilizo kwenye Agano Jipya?

(2) Je, Wakristo wanapaswa kutii sheria zote za Mungu zilizo kwenye Agano la Kale?

(3) Ikiwa si lazima kwa Wakristo kutii sheria zote za Mungu, Je, utajuaje ni sheria gani utakazotii na ni zipi utakazopuuza?

Lengo letu kuu la kujadili maswali haya si kupata jibu bora kwa kila swali. Badala yake, tunataka kuwapa nafasi ya kutoa maoni yao juu ya mada hii na kuona maswala kadhaa tutakayojadili katika somo hili. Tumia muda mfupi kwa majadiliano haya ili usitumie muda mwingi wa darasa. Tutarejelea maswala haya matatu baadaye kwenye somo.

Ikiwa kila mwanafunzi atakubali kuwa tunapaswa kutii sheria zote za Mungu, basi wasomee sheria moja au mbili zifuatazo za Agano la Kale (tazama ukurasa 20 katika Mwongozo wa Mwanafunzi) na uwaulize ikiwa wanatii sheria hizi. Kama hawazitii, waulize ni kwa nini.

**Walawi 11:26-27 BibliaTakatifu (SUV)**

**Kila mnyama aliyepasuliwa ukwato, naye hana kwato mbili, wala hacheui, huyo ni najisi kwenu; kila agusaye wanyama hao atakuwa ni najisi. 27 Tena kila mnyama aendaye kwa vitanga vyake, katika hao wanyama wote waendao kwa miguu minne, hao ni najisi kwenu; awaye yote atakayegusa mizoga yao, atakuwa ni najisi hata jioni.**

(Inajumuisha wanyama wengi, kama vile paka, mbwa na sungura)



**Walawi 20:9 BibliaTakatifu (SUV)**

**Kwa maana kila mtu amlaaniye baba yake au mama yake hakika atauawa, amemlaani baba yake na mama yake; damu yake itakuwa juu yake.**

Uliza ikiwa wangekuwa hai hii leo ikiwa sheria hii ya Walawi 20:9 ingetekelezwa walipokuwa watoto wadogo.

**Walawi 20:10 BibliaTakatifu (SUV)**

**Na mtu aziniye na mke wa mtu mwingine, naam, yeye aziniye na mke wa jirani yake, mtu mume aziniye, na mwanamke aziniye, hakika watauawa.**

**Walawi 19:27 BibliaTakatifu (SUV)**

**Msinyoe denge pembe za vichwani, wala msiharibu pembe za ndevu zenu.**

**Kumbukumbu la Torati 23:12-13 BibliaTakatifu (SUV)**

**Tena uwe na mahali nje ya kituo, kwa kutokea nje; 13 nawe uwe na jembe dogo katika silaha zako; napo uotamapo nje uchimbe kwa lile jembe, na kugeuka na kukifunika kikutokacho.**

**5. Jadili Hoja A, "Aina za sheria za Mungu"**
**(5 -15 dakika) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 21-22**

Waeleze wanafunzi wako kuwa Biblia ina sheria tofauti tofauti. Sheria za Mungu zinaweza kugawanywa angalau kwa makundi manne yafuatayo. (Ikiwa unahisi kuwa kuna makundi mengine muhimu, ongeza.)

(l) Sheria za afya

(2) Sheria za serikali ya raia kwa taifa la Israeli

(3) Sheria za kidini

(4) Sheria za maadili

Itakuwa bora kusisitiza hoja iliyotolewa kwenye ukurasa wa 21 wa Mwongozo wa Mwanafunzi.

> Vikundi hivi vine vinaonekana kuwa rahisi, lakini kwa kweli, sheria zingine zinaweza kutoshea katika vikundi viwili. Kikundi cha mwisho-sheria za maadili - pia ni shida. Kwa kweli, kila sheria katika Biblia ina suala la maadili lililofungamanishwa nalo. Makundi haya manne yameundwa na mwanadamu. Hautapata kifungu katika Biblia ambacho kinavunja sheria hizi katika sehemu hizi nne.
>
> *Nukuu kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa 21*



Eleza kusudi la kila kundi la sheria kwa watu wa Mungu. Toa mifano kadhaa ya sheria zifaazo katika kikundi.

**1. Sheria za Afya**

Vitabu vya Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu, na Kumbukumbu la Torati katika Agano la Kale vimejazaa sheria nyingi tofauti ambazo zinahusiana moja kwa moja na kudumisha afya njema. Kumbukumbu la Torati 23:12-13 iliyonukuliwa hapo juu ni mfano mmoja. Nyingi ya sheria hizi pia hutoa kanuni za kina kuhusu matibabu ya aina tofauti za magonjwa. S. I. McMillen, ambaye ni daktari wa matibabu, ameandika kitabu kizuri kiitwacho, **None of These Diseases** (Flemming H. Revell Publ. Co). Anaeleza usahihi wa matibabu wa sheria za Agano la Kale. Unaweza kusoma kitabu hiki kish ukaona jinsi sheria hizi zinavyofaa kitabibu leo.

**2. Sheria za kiserikali kwa raia wa taifa la Israeli**

Sheria nyingi katika vitabu vya Kutoka hadi Kumbukumbu la Torati zilipewa Wayahudi ili kuanzisha kanuni ya kisheria kwa taifa la Israeli. Huenda ni kati ya Wayahudi milioni moja na tatu walioondoka Misri chini ya uongozi wa Musa. Umati huu wa watumwa wa zamani ilibidi sasa uanzishe serikali ili kushikilia taifa lao jipya pamoja na kutoa uongozi na huduma zote zinazohitajika. Nyingi ya sheria hizi zilishughulikia jinsi ya kutatua migogoro, uuzaji na upangishaji wa ardhi, kutoza riba, utunzaji wa mayatima, n.k.

**3. Sheria za dini**

Sheria nyingi za Agano la Kale zilihusiana na mazoea ya dini ya Kiyahudi. Mafunzo na majukumu ya makuhani na Walawi, aina tofauti za dhabihu za wanyama na chakula, likizo ya kidini, haya ndiyo maswala makuu yanayoshughulikiwa na sheria hizi.

**4. Sheria za maadili**

Sheria za maadili za Mungu mara nyingi huelezewa kama zile sheria za wakati ambapo zinahusika na mahusiano ya watu. Amri Kumi (Kutoka 20:1-17) na sheria mbili kuu katika Biblia (Luka 10:27) ni mifano ya sheria za maadili za Mungu. Sheria za maadili za Mungu zinaweza kutiiwa katika utamaduni wowote, taifa, kipindi cha wakati, na mtu yeyote, bila kujali ni asili gani ya kiuchumi au elimu. Unganisha mstari mkuu na sehemu hii ya somo.

Sisitiza tena kuwa kila sheria katika Biblia ina maadili ndani yake. Kila sheria katika makundi mengine matatu, ina sehemu ya maadili. Hata hivyo tumeita kikundi hiki “sheria za maadili” ili kujaribu kutofautisha vikundi anuwai vya sheria.

3

**6. Ni sheria gani za kutii (Dakika 3-5)**

Sasa uliza tena swali hili: **Je, Mkristo anapaswa kutii sheria zipi za Mungu katika Agano la kale na Agano jipya?** Kisheria, Wakristo hii leo hawajafungwa kwa sheria yoyote ya Agano la Kale. Sheria za kiraia zinazodhibiti muundo wa kiserikali wa taifa la Israeli hazitumiki kwa Wakristo leo. Sheria zinazodhibiti mambo ya kidini ya Wayahudi zilibuniwa kuwaonyesha njia ya kuwasiliana na Mungu. Yesu alikuja kutimiza sheria hizi za Agano la Kale na kuleta njia mpya ya kuabudu.
(Tazama Mathayo 5:17-20)

Kitabu cha Waebrania pia kinatoa ufafanuzi wa kina kuonyesha sheria za Agano la Kale kuhusu dhabihu za wanyama na mambo yote yanayohusiana na dini hayahitajiki tena.

Sheria za afya zilikuwa sehemu ya sheria za taifa la Israeli, ni sawa na jinsi serikali zetu za sasa zinavyopitisha sheria zinazohusiana na afya. Ingawa hatujalazimishwa kutii sheria hizi zote za Agano la Kale, baadhi ya sheria hizi zinatoa miongozo bora sana ya kudumisha afya bora. S.I. McMillen anaotoa mifano mingi katika kitabu chake,
**None of These Diseases.**

**7. Tanguliza Hoja B. “Mjadala kuhusu nisheria zipi tunapswa kutii leo” (dakika 5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 22-24**

Maelezo ya jumla ya makundi 4 ya sheria za Mungu yanatutayarisha kwa suala la pili tulilotanguliza kwa “Zoezi la utangulizi wa somo”. Unaporejelea suala hili tena— mjadala kuhusu sheria tunazopaswa kutii hii leo — amua ni muda gani utatumia, kuendeleza kilichoanzishwa katika sehemu ya kwanza ya somo.

Kuwa mwangalifu sana na wakati wako. Suala kuu kwa leo si kutumia wakati wako wote darasani kujadili haya. Mjadala huu ni sehemu tu ya msingi wa suala kuu zaidi - jinsi ya kujua na kutii kanuni kutoka kwa Mungu ambazo ni chanzo cha sheria katika Biblia. Angalia hoja ya 11 katika mpangilio wa somo la leo.

Hatujaribu kuzua mabishano, lakini wanafunzi wetu wanapaswa kujua kwamba Wakristo na wasio Wakristo wote wana maoni tofauti kuhusu suala hili la sheria tunazopaswa kutii hii leo. Hii pia ndio sababu ya mgawanyiko kati ya madhehebu ya kanisa.

Lengo letu leo si kusema ni nani wa kweli na nani amekosea. Tunataka kuwafahamisha kuwa hili ni suala lenye utata, na tuwasaidie kuona jinsi wanavyoweza kufanya uamuzi bora katika sehemu hii ya maisha yao.

Waelekeze wanafunzi wako kwenye ukurasa wa 22 katika Mwongozo wa Mwanafunzi na uwaeleze kuwa utata huu si jambo geni — Adamu na Hawa walikumbana na haya katika Bustani ya Edeni. Shetani alimdanganya Hawa kuamini kuwa hakuna ubaya wowote wa kutotii sheria za mungu. Tunapaswa kujua kwamba Shetani atafanya kila awezalo kutudanganya kama alivyomdanganya Hawa.

Hata hivyo, tunapaswa kuwa waangalifu ili tusiwe na mtazamo kuwa mtu yeyote ambaye hakubaliani na msimamo wetu kuhusu suala hili anadanganywa na shetani.

Waambie wanafunzi wako kwamba tutaangalia kwa ufupi misimamo tofauti,
na tuone ni nini inasema kuhusu utiifu kwa Mungu.

**8. Jadili Msimamo wa 1. "Wakristo leo hii wanapaswa kutii Sheria zote za Agano la Kale" (dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 23**

Sisistiza kuwa Wakristo wengi leo hawashikilii msimamo huu. Hata hivyo maandiko katika Mathayo 5:17-19 yanaweza kumchanganya sana Mkristo mpya.

Jadili na wanafunzi wako mfano kutoka Matendo 15:24-29 pale ambapo viongozi wa kanisa la Agano Jipya walishughulikia suala hili la sheria za Agano la Kale.

Pia waelekeze wanafunzi wako kwa aya ya mwisho katika Mwongozo wa Mwanafunzi kuhusu msimamo ulio tofauti kuhusu sheria za Agano la Kale. Onyesha utata uliotokana na msimamo huu - kila mtu anapaswa kuamua ni sheria gani atatii sasa, na ni gani atapuuza. Je, watatumia vigezo gani, na ni nani atasema ni sawa au sio sawa?



> Tofauti ya msimamo huu ni kwamba Wakristo wanahitajika kutii sheria kadhaa za Agano la Kale, lakini si zote. Hii inatuweka kwa wakati mgumu wa kuamua ni sheria gani za kutii na ni zipi za kupuuza.
>
> *Nukuu kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa 23.*

**9. Jadili Msimamo wa 2. "Wakristo wanahitaji kutii sheria za Mungu katika Agano Jipya" (3-5 dakika) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 23-24**

Watu wengine wanaamini kwamba hatupaswi kujishughulisha na sheria za Agano la Kale hii leo. Wanatetea msimamo huu kwa kusema kuwa Yesu alipokuja miaka 2000 iliyopita, alikuja kuanzisha agano jipya, na kwa hivyo agano la zamani la Agano la Kale - na sheria ambazo ni sehemu ya agano hilo la kale – halituhusu hii leo.

Watu wengine hawaoni thamani nyingine ya Agano la Kale isipokuwa kutoa hadithi za kuvutia. Hii ni tofauti sana na watu wengi ambao wanathamini sana vitabu vyote 66 vya Biblia.

**10. Jadili Msimamo wa 3. "Mahali pa kuanzia kwa Wakristo wapya" (dakika 2-3) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 24**

Rejea ukurasa wa 24 katika Mwongozo wa Mwanafunzi kwa habari kuhusu msimamo huu. Tunapaswa kuwa waangalifu sana tusigeuze mjadala kuwa wa kisheria. Lengo letu halisi ni kujifunza jinsi ya kumtii Mungu — si jinsi ya kuepuka kutii sheria Zake.

Wakristo wapya wanapaswa kuanza kuliona swala hili kama – nataka kuwa na uhusiano wa kibinafsi na Yesu. Ninataka kumwonyesha kwamba ninampenda. Kumtii Mungu ni mojawapo ya njia bora za kuonyesha kwamba ninampenda.

Mahali pa kuanzia ni upendo — si mjadala wa kisheria juu ya sheria.

Tumia utangulizi huu mfupi kuendelea na sehemu ya pili ya somo hili ambayo ni sehemu muhimu kwa darasa la leo. Tunapaswa kutii kanuni zinazohusiana na sheria za Mungu. Huu ni mwongozo unaohusiana na sheria zote za Mungu.

**11. Jadili Hoja C. Tii kanuni zinazoshikilia sheria za Mungu (dakika 10-20) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 24-26**

Jadili sheria ambazo Wakristo wanapaswa kutii (Hoja #6 -10 kwenye mpangilio huu wa somo) kutanguliza sehemu ifuatayo ya somo. Tunapaswa kutii kanuni ambazo ni chanzo cha sheria za Mungu. Huu ni mwongozo ambao unahusiana na sheria zote za Mungu.

Kila sheria ya Mungu inategemea kanuni ya maisha. Tunaweza pia kusema kwamba kila sheria ya Mungu inategemea kanuni ya maadili.

3

Kwa kila sheria ya Mungu kuna sababu inayofaa mpango wa mungu wa kuishi maisha matakatifu. Tunapaswa kujifunza jinsi ya kujua kanuni ambazo ni msingi wa kila sheria na kujifunza jinsi ya kutumia kanuni hizo kwa hali tunazokumbana nazo hii leo. Hivi ndivyo tutajua jinsi ya kukabiliana na hali kama vile uvutaji wa sigara, kutumia dawa za kulevya, kuendesha gari kwa kasi, nk.

Chukua muda sasa kujadili baadhi ya sheria katika Biblia — kutoka Agano la Kale na Agano Jipya. Unaweza kugawa darasa lako katika vikundi vidogo na kila kikundi kiangalie sheria moja. Baada ya kumaliza kazi yao, waache waripoti matokeo yao kwa darasa zima.

Kwa kila sheria kutoka kwa Biblia, zungumzia maswala haya matatu.

1. Kwanza angalia sheria inavyosema.
2. Kisha jadili msingi wa kanuni za sheria hiyo. Kanuni hii inatuambia nini kumhusu Mungu na mfumo wake wa thamani?
3. Kanuni hii inawezaje kutumika katika maisha yangu ya kila siku kunisaidia kukabiliana na matatizo na changamoto ninazokumbana nazo kila siku?

**Mfano wa Kwanza: Kumbukumbu la Torati 23:12-13 kuhusu matumizi ya choo.**

**Kumbukumbu la Torati 23:12-13 BibliaTakatifu (SUV)**

**Tena uwe na mahali nje ya kituo, kwa kutokea nje; 13 nawe uwe na jembe dogo katika silaha zako; napo uotamapo nje uchimbe kwa lile jembe, na kugeuka na kukifunika kikutokacho.**

1. **Sheria inasema nini:** Inatoa maagizo ya jinsi ya kutumia vizuri “choo cha nje.”
2. **Kanuni inayohusiana na sheria hii:** umuhimu wa kuwa na mazingira safi.

Hata leo katika sehemu zingine za ulimwengu, miongozo ya kimsingi ya usafi hupuuzwa na matokeo huwa mabaya. Magonjwa huenea haraka wakati kinyesi kinachafua maji ya kunywa na vyakula. Kanuni ya sheria hii ya Agano la Kale ni kwa watu kuishi katika mazingira safi na kutoa njia bora ya kutupa dutu hili lililojaa viini. Pia tunapozika kinyesi, huoza na hubadilika na kuwa mbolea ya mimea na huuwa viini vinavyosababisha magonjwa.

3. **Kutumia kanuni hii maishani mwangu leo:**

   a. Ninapaswa kuwa mwangalifu na kutumia njia nzuri za usafi ninapojisaidia. Ninapaswa kuvuta maji ya choo ninapomaliza kukitumia.

   b. Ninapaswa kunawa mikono yangu baada ya kutumia choo.

   c. Ninapaswa kusafisha mahali alipotumia mbwa wangu, haswa ikiwa ninaishi mjini-kinyesi chao pia kinaweza kusambaza viini na magonjwa.

Kanuni hii pia inaweza kutumika kuweka kituo cha kutibu maji taka ambacho hutibu maji taka na kuondoa viini kabla ya kuyarudisha kwenye mito.



Inaweza pia kutumiwa kuweka mfumo wa kusafisha maji ambao hutibu maji yote ya kunywa ili kuhakikisha kuwa ni safi kabla ya watu kuyanywa.

**Mfano wa Pili: Mathayo 5:21-22 Mauaji dhidi ya hasira**

> **Mathayo 5:21-22 BibiliaTakatifu (SUV)**
>
> **Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, Usiue, na mtu akiua, itampasa hukumu. [22] Bali mimi nawaambieni, Kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu; na mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza; na mtu akimwapiza, itampasa jehanum ya moto.**

Katika mfano huu, Yesu anaonyesha kanuni ambazo ni chanzo cha sheria za Mungu katika Agano la Kale. Unaposoma Mahubiri Mlimani, Yesu anatoa mifano kadhaa ya jinsi watu katika nyakati hizo walivyokosea na kishindwa kutumia kanuni hii vizuri katika maisha yao.

1. **Sheria inasema nini:** Usiue.
2. **Kanuni inayohusiana na sheria hiyo:** Heshimu maisha ya mwanadamu. Waheshimu watu wengine.
3. **Kutumia kanuni hii maishani mwangu leo:** Usimkasirikie ndugu yako.

Ikiwa una muda wa kutosha, unaweza kujadili mifano mingine ya sheria za Mungu na uelekeze darasa lako kwa hatua hizi 3 za kuchagua kanuni ambazo zinaweza kutumika maishani mwao hii leo. Unaweza pia kuangalia maswala kadhaa ya kisasa—kama vile kuendesha gari kwa kasi—ambayo hayajashughulikiwa haswa kwenye Biblia, na utafute sheria ambayo ina kanuni inayohusiana moja kwa moja na suala hilo. Suala la uendeshaji wa gari kwa kasi, Warumi 13:1-2 ni mfano mmoja — angalia ukurasa wa 25 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

3

**Mfano wa Tatu: 1 Wakorintho 9:9 na 1 Timotheo 5:17-18: Kulisha wanyama wako na kuwatunza wahudumu wako**

**1 Timotheo 5:17-18 BibliaTakatifu (SUV)**

**Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu; hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha.**
**18Kwa maana andiko lasema, Usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka. [1] Na tena, Mtenda kazi astahili ujira wake. [2]**

Tanbihi: 1. Kumb. 25:4, 2. Luka 10:7

Katika Agano Jipya, Paulo alitumia sheria ya Agano la Kale ambayo inahusiana na utunzaji wa ng'ombe wako na alitumia kanuni ya sheria hiyo kueleza ni kwa nini makanisa yanapaswa kuwalipa wachungaji wao.

Ananukuu Kumbukumbu la Torati 25:4 mara mbili (l Wakorintho 9:9 & 1 Timotheo 5:18). Angalia mistari iliyo karibu na mstari huu ili kuona maoni ambayo Paulo anatoa kwa kutumia sheria hii ya Agano la Kale.

Kwa kutumia mifano hii, wafahamishe wanafunzi wako kuwa hizi si sheria halali ambazo ni lazima wazitii. Inahusu kufahamu kanuni za Mungu ili kuwa na maisha yenye mafanikio. Nimeanua kuzitii kanuni za Mungu maishani mwangu kama nielewavyo-nimeamua kuzitenda kila siku—kwa sababu nataka kufanya hivyo! Ni njia ya kuonyesha upendo wangu kwa Mungu.

Njia nyingine ya kuangalia sehemu hii yote ya somo la leo ni kuiona kama njia moja ya kutii Amri kuu katika Biblia. Nitamwonyeshaje Mungu kwamba ninampenda? Ninapofahamu kanuni ambazo ni chanzo cha sheria ya Mungu katika Biblia, na kujaribu kutimiza kanuni hizo katika maisha yangu ya kila siku-hii ni njia nzuri ya kumwonyesha Mungu kwamba ninampenda.

## 12. Roho ya sheria dhidi ya barua ya sheria (dakika 5)

Kutii kanuni za sheria kunahusiana sana na suala lingine linalojadiliwa katika Biblia. Katika sehemu mbalimbali tunaambiwa tutii roho ya sheria; na sio tu barua ya sheria. Utiifu wenye busara unamaanisha kwamba tunaangalia kwa makini sheria ambazo Mungu ametupatia ili kufahamu sababu kuu ya kuwa na kila sheria.

Yesu aliwakosoa vikali Mafarisayo kwa tafsiri yao ya kisheria ya Agano la Kale na wakati huo huo wakipuuza kanuni za Mungu ambazo ni msingi wa sheria hizi zote. Katika Mathayo 23:23 Yesu aliwaambia watii sheria zinazohusiana na zaka, n.k., lakini pia watii kanuni ambazo ni chanzo cha sheria hizi.

Katika Mahubiri Mlimani, Yesu alifanya jambo kama hilo kwa kunukuu sheria ya Agano la Kale au mila ya Kiyahudi na kisha akaonyesha kanuni ambayo ni chanzo cha sheria hiyo ilihusisha maisha yenye vikwazo au matakatifu. Tazama Mathayo 5:21-48.

**13. Zoezi la 4 Mwongozo wa Somo, "Kuangalia kwa makini sheria moja" (dakika 10-15)**

Zoezi la 4, *"Kuangalia kwa makini sheria moja,"* katika Mwongozo wa somo linaweza kutumika wakati huu wa somo. Wape wanafunzi kadhaa fursa ya kusimulia yale waliyokumbana nayo walipokuwa wakikamilisha zoezi hili. Unaweza pia kutumia zoezi hili kwa somo 4 wakati tunajadili matokeo ya kutii na kutotii sheria za Mungu. Angalia hoja ya 10 katika mpangilio wa somo kwa mwalimu kwa somo la nne.

**14. Jadili Hoja D. "Mapenzi ya Mungu" ni nini?"**
**(Isiyo ya lazima: Dakika 10-15 au kipindi chote cha darasa)**
**Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa 26-27**



Kufanya mapenzi ya Mungu ni njia nyingine ya kutii amri kuu katika Biblia. Maada ya mapenzi ya Mungu ni suala pana na mara nyingi lenye utata katika maisha ya Kikristo. Unaweza kulizungumzia kwa kifupi leo, au uwe na kipindi tofauti cha darasa na ujadili kwa kina zaidi.

Ukurasa wa 26-27 wa Mwongozo wa Mwanafunzi unatoa orodha ya masuala 8 makubwa ambayo ni mapenzi ya Mungu kwa kila mtu. Kujifunza kuhusu mapenzi ya Mungu kunafaa katika kozi hii ya utiifu kwa Mungu kwa sababu ni sehemu ya maisha ya Kikristo ambayo inahusisha utiifu.

Tunaweza kusema kuwa 95% ya mapenzi ya Mungu kwa kila Mkristo yameelezwa katika Biblia. (Tazama ukurasa wa 26-27 wa Mwongozo wa Mwanafunzi kwa mifano.) Wakati mwingine Wakristo hufanya mapenzi ya Mungu kuwa yenye utata zaidi kuliko ipasavyo. Ikiwa tungefanya yale Biblia inatuambia tufanye, wengi wetu wangekuwa na muda mfupi sana wa kuwa na wasiwasi juu ya 5% iliyosalia ya mapenzi ya Mungu kwa maisha yetu.

Eleza kwamba Mungu hufunua mipango yake kwa kila Mkristo achaguwavyo, si kila wakati mtu anapomuomba. Kwa kawaida hatakuambia kile Anachotaka ufanye miaka 10 kabla ya wakati. Wahimize wajipanga mapema, lakini wawe na mtazamo unaoweza kubadilika, wakifahamu kuwa Mungu ana haki ya kubadilisha mipango yao ikiwa Atataka. Tazama Yakobo 4:13-16.

**15. Imani ya Kibinafsi na Masilahi ya Kibinafsi**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa 27-28**

Unapojadili mapenzi ya Mungu, unaweza pia kujadili mada ya imani ya kibinafsi. Roho Mtakatifu mara nyingi huwaonyesha watu kuhusu mambo fulani ambayo hataki wafanye. Kwa mfano, watu wengine wana imani za kibinafsi juu ya kunywa divai, kwenda kwenye sinema, kuvaa mavazi ya aina fulani, au jinsi ya kutumia pesa zao. Imani hii ya kibinafsi ni sehemu muhimu ya mapenzi ya Mungu kwa mtu huyo.

Njia nyingine ya kuelezea usadikisho wa kibinafsi ni kuuona kama "mpaka wa kibinafsi" ambao Mungu amemwekea mtu huyo. Hata hivyo, hakikisha kuwa umefafanua hoja iliyo katika Mwongozo wa Mwanafunzi—Mungu kamwe hatatupatia uthibitisho binafsi ambao unasema tufanya jambo ambalo haliruhusiwi na mojawapo ya sheria za Mungu. Imani ya kibinafsi kutoka kwa Mungu huweka mipaka mikali kwa mtu huyo kuliko sheria katika Biblia.

Onyesha umuhimu wa kila mmoja wetu wa kuheshimu imani ya kibinafsi ya wengine. Lakini wakati huo huo tusilazimishie wengine usadikisho wetu wa kibinafsi. Soma 1 Petro 2:16 na uone jinsi mapenzi ya Mungu yanahusiana na sheria za Mungu.

Kwa Wakristo wapya suala la imani ya kibinafsi kutoka kwa Mungu dhidi ya masilahi ya kibinafsi linaweza kuwatatanisha. Taja kuwa Wakristo wengi — vijana na wazee — hawatofautishi sehemu hizi mbili.

Ikiwa mtu hapendi kahawa — hiyo si imani ya kibinafsi kutoka kwa Mungu — hilo tu ni chaguo la kibinafsi la kinywaji. Hakuna ubaya wowote wa kuchukia kahawa, lakini hiyo haina maana ya moja kwa moja kwamba Mungu ndiye chanzo cha chaguo hili la kibinafsi.



Tunapaswa kuwasaidia wanafunzi wetu kuelewa umuhimu wa kutoingilia mjadala wa kisheria wa imani za kibinafsi. Sisitiza kwamba ni imani za kibinafsi.

**16. Kutumika Binafsi (dakika 5-10)**

Angazia kutumika binafsi kwa leo katika utiifu wa sheria za Mungu. Wahimize wachague sheria moja ya Mungu ambayo inahusiana na sehemu ya maisha yao ambayo inahitaji kukua. Kuanza kwa sheria moja kati ya sheria mbili kuu ni jambo nzuri.

Pia wahimize kuchukua muda wa kufahamu kanuni ambayo ni chanzo cha sheria za mungu. Wanapokabiliwa na hali ambayo hawajui sheria yoyote maalum ya Mungu ambayo inawaeleza jinsi ya kukabiliana na hali hiyo, wanapaswa kuchagua kanuni ya Mungu inayoweza kuwasaidia kujua la kufanya katika hali hiyo. Wakumbushe kwamba tuna Roho Mtakatifu kama mwalimu na kiongozi wetu. Tunahitaji kuwa wenye busara kwa dhamiri zetu kwani Mungu huongea nasi kupitia kwa dhamira.

**17. Kazi**

A. Mwishoni mwa kipindi cha darasa, wape mtihani kutoka Yohana 13:34-35.

B. Sahihisha Mwongozo wa Somo zoezi la 4,*"Kuangalia kwa makini sheria moja,"* ikiwa uliutumia katika somo la leo.

C. Waambie wanafunzi wasome Sura ya 4 na 5 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi ili kujiandaa kwa kipindi kifuatacho cha darasa

**18. Tathmini ya Somo**

Orodhesha maoni yako ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu gani ziliokuwa bora zaidi?
Ni sehemu gani zilizokuwa ngumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 4
# Matokeo ya kumtii na kutomtii Mungu

## 1. Kweli Kuu Ya KiBblia

Ninapaswa kufikiria kwa makini kuhusu matokeo ya kumtii au kutomtii Mungu katika maisha yangu ya kila siku.

## 2. Mstari Mkuu:

Mithali 13:13 BibliaTakatifu (SUV)

Kila alidharauye neno hujiletea uharibifu; Bali yeye aiogopaye amri atapewa thawabu.

## 3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili



Sura ya 4 na 5 katika Mwongozo wa Mwanafunzi inaendana na somo hili. Zoezi la 3, *"Matokeo ya kutii na kutotii,"* na Zoezi 4, *"Kuangalia kwa makini sheria moja,"* katika Mwongozo wa Somo pia inaweza kutumika kwa pamoja na somo hili.

## 4. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5-10)

Chagua moja kati ya visisimuzi viwili vifuatavyo kuanzisha somo hili.

### A. Kama ningekuwa Mungu.

Mwambie kila mwanafunzi aandike maoni yake vile angekamilisha sentensi hizi.

(1) Ningekuwa Mungu, hivi ndivyo ningewatuza watu wanaonitii.

(2) Ningekuwa Mungu, hivi ndivyo ningewaadhibu wenye dhambi (wasio Wakristo) ambao hawanitii.

(3) Ningekuwa Mungu, hivi ndivyo ningewaadhibu Wakristo wasiponitii.

(4) Ningekuwa Mungu, hivi ndivyo ningewashawishi watu wanitii.

Baada ya wanafunzi kuandika maoni yao, wape fursa ya kuwasilisha maoni yao darasani. Kusudi kuu hapa ni kuangazia mada kuu ya kipindi cha leo cha darasa, kwa hivyo hatutafuti jibu lolote sahihi au lisilo sahihi.

### B. Kuwa Askari wa Mungu

Unaweza kuwapa wanafunzi wawili au watatu nafasi ya kuigiza au urekodi video ya mchezo wa kuigiza kisha ucheze rekodi hapo mwanzoni mwa kipindi cha darasa. Mpe nafasi mwanafunzi mmoja au wawili ya kujitambulisha kama askari wa Mungu.

Wanawajibika kuona kwamba watu wanazawadiwa kwa kutii sheria za Mungu. Pia wamepewa kazi ya kuwashika watu ambao hawatii sheria za Mungu na kuripoti kwa Mungu. Lazima pia wamwadhibu mtu huyo jinsi Mungu aonavyo ni sawa kwake.

Wape askari fursa ya kusimulia yale waliyoyashuhudia hivi karibuni.

**5. Orodha ya matokeo ya kutii na kutomtii Mungu (dakika 10-15)**

Unda orodha mbili kwenye ubao au kwenye karatasi kubwa. Andika orodha moja ya matokeo ya kumtii Mungu, na uandike orodha nyingine ya matokeo ya kutomtii Mungu. Unaweza kuacha darasa zima lifanye zoezi hili kwa pamoja kama kikundi kimoja kikubwa na kisha mtu mmoja aandike orodha ya kila tokeo. Au unaweza kugawanya darasa katika vikundi vidogo na kila kikundi kipewe karatasi mbili na kalamuili waandike orodha zao.

Wahimize kuandika kifungu cha maandiko kwa kila tokeo wanaloorodhesha. Wanaweza kutumia majibu kutoka kwa Zoezi la 3 kutoka kwa Mwongozo wa somo kuandika orodha hizi.

Baada ya kuunda orodha zao, kila kikundi kitoe ripoti kwa darasa juu ya matokeo yao. Orodha hizo mbili zinaweza kuwa na matokeo mengi ambayo ni tofauti. Unapozungumza zaidi juu ya jambo hili leo, ndivyo itakavyokuwa wazi zaidi kwa kila mtu kwamba ni bora kumtii Mungu. Matokeo ya kumtii Mungu siku zote huonekana kuwa bora kuliko kutomtii Mungu.

4

Unapomaliza mjadala huu, sisitiza kuwa mara nyingi tunashindwa kuona athari ya matendo yetu ya utiifu au ya kutotii. Ikiwa bado haujafanya hivyo, waelekeze wanafunzi kwenye orodha ya watu katika ukurasa wa 29 katika Mwongozo wa Mwanafunzi, na uonyeshe jinsi watu hawa wameathiriwa na matendo yetu ya utiifu au ya kutotii.

**6. Kuangalia kwa makini mifano kadhaa ya kibiblia ya kumtii Mungu na kutomtii Mungu (dakika 5-10)**

Mwongozo wa Mwanafunzi unachunguza kwa undani mifano miwili ya Agano la Kale ya kumtii Mungu — Yusufu na Shadraka, Meshaki, na Abednego. (Tazama ukurasa wa 30) Unaweza kupitia mfano mmoja au yote mawili ili kuwasaidia wanafunzi wako kuona matokeo ya kumtii Mungu.

Mwongozo wa Mwanafunzi pia una mfano wa kisasa wa Brian wa kumtii Mungu (kurasa 30-31). Tunachopaswa kusisitiza katika darasa la leo ni kwamba Mungu anaona matendo yetu ya utiifu na kutotii. Ameahidi katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati 11:26-28 kutubariki au kutuadhibu kwa matendo yetu.

Katika Sura ya 5 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi, kuna mifano ya kibiblia iliyotolewa ya kutomtii Mungu — Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni, na Mfalme Daudi na Bathsheba. (Tazama ukurasa wa 33-34)

Kuna mifano mingine mingi ya kibiblia ya kumtii Mungu na kutomtii Mungu ambayo inaweza kutumika katika somo hili. Tazama ukurasa wa 31 kwa orodha ya maandiko mengine yanayozungumza kuhusu matokeo ya utiifu na ukurasa wa 38 kwa orodha ya maandiko mengine yanayozungumzia matokeo ya kutotii.

Sisitiza umuhimu wa kuuliza swali: “Ninaweza kujifunza nini kutokana na utiifu au kutotii kwa wengine?” Ni jambo la maana kwetu kujifunza kutokana na mafanikio na makosa ya wengine — badala ya kujifunza kutoka kwa maisha yetu wenyewe.

**7. Jadili Hoja B. Maneno manne muhimu yanayohusiana na kutotii (dakika 5-10) Mwongozo wa Mwaanafunzi, ukurasa wa 35-38**

Kurasa 35-38 za Mwongozo wa Mwanafunzi zinazungumzia maneno manne makuu yanayohusiana na kutotii:

1. Matokeo ya asili
2. Nidhamu
3. Adhabu
4. Kisasi

Unaweza kumpa kila mwanafunzi neno moja kati ya maneno haya 4 makuu kabla ya kipindi hiki cha darasa, na uwape wanafunzi fursa ya kutoa ripoti fupi darasani. Wanaweza kujumuisha mifano ya kibiblia na ya kisasa inayoonyesha neno lao kuu.

Neno la kwanza lililoorodheshwa, matokeo ya kawaida, linahusiana moja kwa moja na utiifu na ukosefu wa utiifu wa . Maneno mengine 3 makuu yanahusiana zaidi na kutotii.



Unapojadili suala la "adhabu," unapaswa kueleza kwa kifupi kuwa katika darasa letu la leo, tunatumia maana ya juu wa adhabu, na kutofautisha na nidhamu. Hata hivyo, katika nyakati za Biblia na leo, neno adhabu mara nyingi lilitumiwa kwa maana ya ndani inayojumuisha dhana ya nidhamu kama inavyowasilishwa katika somo hili.

Unapomaliza sehemu hii ya somo, hakikisha kuwa wanafunzi wako wanaelewa tofauti kati ya maneno haya manne ambayo yanahusiana na matokeo ya kutotii.

Unapojadili maneno haya manne, jaribu kutoa mifano kwa kila neno na jinsi yanavyohusiana na kumtii na kutomtii Mungu. Taja kuwa adhabu au nidhamu ambayo Mungu hutoa kila wakati ni ya haki. Mungu ni Mungu wa haki. Kila mtu hupata "haki" kwa Mungu wakati anapotii au kutotii mmoja ya sheria za Mungu.

**8. Jadili Hoja C, "Je, Mtazamo wa Mungu ni nini kwa watu wasiotii sheria zake?" (Dakika 5-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 39-41**

Mwongozo wa Mwanafunzi unatoa nyenzo za msingi za majibu 5 kwa swali hili. Kabla ya kuingia kwenye mjadala wa yale Mwongozo wa Mwanafunzi unasema juu ya swala hili, unaweza kuuwauliza wanafunzi wako swali hili ili kupata maoni yao.

Wanafunzi wako wanaweza kuwa na maoni tofauti juu ya suala hili kulingana na mahali wanapotoka. Jaribu kuepukana na kuwamazungumzo ya nadharia na theolojia, yafanye kwa vitendo, na utumie mifano halisi ya maisha, pengine ya kisasa au kutoka kwa Biblia.

Unapoendelea na majadiliano haya, tunataka wanafunzi wetu waanze kuelewa umuhimu wa kuwa na mtazamo kama wa Mungu kuhusu dhambi. Hii inamaanisha kuwa tunapaswa kufanya juhudi ya kubadilisha imani zetu juu ya mambo fulani kuhusu dhambi. Hapo zamani wanafunzi wako pengine hawakuona ubaya wowote wa kushiriki kwa mambo fulani — lakini kwa kuwa sasa wanataka kumtii Mungu, wanapaswa kuyaona jinsi Mungu anavyoyaona.

**9. Unaweza kuchukua muda wa kujadili uhusiano kati ya rehema za Mungu na haki Yake.**

Hapa ni njia moja ya kueleza uhusiano huu. Ikiwa mtu atatenda dhambi, na akatae kukubali au kukiri dhambi hiyo, Mungu atatenda haki na kumwadhibu mtu huyo jinsi anavyostahili. Lakini kama mtu atatenda dhambi, na akubali na akiri kwa Mungu, basi Mungu mara nyingi humhurumia. Wakati Mungu anamhurumia, mara nyingi hutoa"hukumu nyepesi" kwa kitendo cha kutotii.

Jambo hili linaonekana wazi katika maisha ya Daudi na Sauli katika Agano la Kale. Sauli alikataa kuungama dhambi zake na Mungu alimwadhibu vikali. David katika miaka yake mingi ya ufalme alifanya dhambi mbaya (kutoka kwa mtazamo wa binadamu) kuliko alivyofanya Sauli. Lakini Daudi alikiri dhambi zake kila mara na mara nyingi Mungu alimwonyesha rehema.

4

Daudi alifunga na kuomba katika 2 Samweli 12 kwa ajili ya mtoto wake hadi alipokufa, aliwaambia watumishi wake baadaye kwamba alifanya hivyo kwa sababu alifikiri Mungu anaweza kumwhurumia na kuyaokoa maisha ya mtoto wake. Daudi alifahamu rehema za Mungu na akajifunza uhusiano wa rehema na kukiri kwa kweli.

Ikiwa mtu atakataa kukiri dhambi zake, basi pengine rehema za Mungu hazitabadilisha mitazamo yake. Lakini nidhamu ya Mungu na adhabu wakati mwingine humfanya mtu kufikia hatua ya kuwa tayari kukiri dhambi zake. Yohana 3:l8-21 inazungumzia hatima inayomngojea mtu ambaye anakataa kuungama dhambi zake na kumwamini Yesu.

**10. Zoezi 4 la Mwongozo wa Somo, "Kuangalia kwa makini sheria moja" (dakika 10-15)**

Zoezi la 4 katika Mwongozo wa somo linaweza kutumika wakati huu.
Waache baadhi ya wanafunzi wazungumzie waliyojifunza wanapokamilisha zoezi hili. Unaweza kuelekeza mjadala kwa matokeo ya papo hapo yaliyotokana na kutii au kutotii wale walio mamlakani. Unaweza pia kutumia mifano ya hivi karibuni ya kibinafsi kueleza matokeo ya kutii au kutotii.

**11. Matumizi binafsi (Dakika 5-10)**

A. Angazia matumizi binafsi ya somo hili kwa kuwapa changamoto ya kumtii Mungu kila wakati. Wahimize kuangalia matokeo ya kumtii Mungu na baraka atakazowaletea wale wanaomtii. Tumia orodha zilizoundwa mwanzoni mwa kipindi cha darasa kutilia mkazo tofauti iliyoko kati ya orodha hizo mbili.

B. Waambie wanafunzi wako waandike maombi kwa Mungu, kumshukuru kwa kuwa Mvumilivu, mwenye upendo, huruma na haki. Wahimize wamwombe msaada na nguvu za kumtii leo na siku zijazo.

C. Wahimize wanafunzi wako kuandika jarida la mifano maishani mwao au maishani mwa wengine walio karibu nao ya matokeo ya kumtii na kutomtii Mungu. Ufahamu huu unaweza kuwa ukumbusho wa kila siku juu ya umuhimu wa kumtii Mungu wanapokabiliwa na majaribu ya kutenda dhambi — ambayo yanamaanisha kutomtii Mungu.

### 12. Kazi

Ikiwa bado haujafanya hivyo, sahihisha Zoezi la 3 kwenye Mwongozo wa Somo, *“Matokeo ya Kutii na Kutotii,”* na Zoezi la 4, *“Kuangalia kwa makini sheria moja”*.

### 13. Tathmini ya Somo

Orodhesha maoni yako ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu gani ziliokuwa bora zaidi?
Ni sehemu gani zilizokuwa ngumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 5
# Mtihani

**1. Utangulizi**

Fanya utangulizi wa somo litakalofuata.

A. Wape Mwongozo wa Somo au Mazoezi yoyote ambayo yanapaswa kukamilishwa kabla ya kipindi cha kwanza cha kozi ifuatayo utakayofundisha.

B. Waelekeze wanafunzi kufungua ukurasa wa mwisho katika Mwongozo wa Somo Lipya. Wanapaswa kupata nakala safi ya ***Orodha ya Kazi za Darasani.*** Wape tarehe za majaribio ya chemsha bongo, Zoezi, na mtihani.

C. Wape Mwongozo wa Mwanafunzi mpya na uwaambie kurasa watakazosoma kabla ya kipindi kifuatacho darasani.

**2. Wape mtihani wa Somo hili.**

**3. Ikiwa hujafanya hivyo bado, rudisha chemsha bongo zote na mazoezi ambayo umesahihisha.**

# Mwongozo wa Mwanafunzi

Mwongozo wa Mwanafunzi Haujajumuishwa kwenye hati hii,
lakini unapatikana katika hati tofauti.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Mwanafunzi.

# Mwongozo wa Somo

Haukujumuishwa kwenye hati hii, lakini unapatikana katika hati tofauti.

.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Somo.

# Mtihani

# Majibu ya mtihani

# Cheti cha Somo

Tazama ukurasa wa 5 wa mwongozo huu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mtihani na cheti.

**Jina**______________________ **Utiifu kwa Mungu**

**Tarehe** ____________________ **Mtihani wa Toleo la 5**

**Darasa** ____________________ ________**Gredi**

**Maswali ya Kweli-Si Kweli** (Alama 2 kwa kila moja)

**Maelekezo:** Weka alama ya ___X_____ ikiwa jibu ni kweli.
Weka alama ya ___O_____ ikiwa jibu si kweli.

1.________Sheria kuu zaidi katika Biblia inatwambia tuwapende majirani sawia na jinsi Mungu anavyotupenda.

2.________Kuzitii sheria za Mungu ni mojawapo wa mambo ya muhimu zaidi unayoweza kuyafanya kama Mkristo.

3.________Mungu anakukasirikia kila mara unapokosa kutii mojawapo ya sheria zake.

4.________Unaweza kutii sheria zote za Mungu na bado usimpende Mungu.

5.________Mojawapo wa mambo muhimu sana ambayo Mungu alituambia tufanye ni kumpenda Yeye.

6.________Mungu anapenda Wakristo peke yao.

7.________Kwa kuwa Biblia haina sheria zozote kuhusu kuvuta sigara, ni sawa kwa Wakristo kuvuta sigara.

8.________Mungu anataka kila mmoja awe Mkristo.

9.________Njia ya pekee ambayo Mkristo anaweza kutambua kile Mungu anataka afanye ni ya Mungu kumpa ishara ya kipekee.

10._______Iwapo ungependa kufaulu katika kutii sheria za Mungu, lazima uwapende viongozi wako.

11._______Mungu hajali mtazamo wako ulivyo. Kile anachojali ni wewe kumtii Yeye.

12._______Mungu anakuadhibu kila mara punde tu unapokosa kutii mojawapo ya sheria zake.

13._______Njia bora zaidi ya kuonyesha unampenda Mungu ni kwa kutii sheria zake.

14._______Mungu anakutaka uwe na mtazamo unaofanya iwe rahisi kwako kutii sheria zake.

**Maswali ya Kweli-Sio Kweli** *(Kuendelezwa)*

15._______Ni rahisi kila mara kutii sheria zote za Mungu.

16._______Ni muhimu sana kwako kuonyesha upendo wa Mungu kwa wengine kuliko kuonyesha upendo wako kwa Mungu.

17._______Wakristo wa leo wanahitajika tu kutii sheria zilizo katika Agano Jipya.

18._______Sababu nzuri zaidi ni kwa nini unapaswa kutii sheria za Mungu ni kukukinga kwenda kuzimu.

**Maswali ya Kuchagua Kati ya Majibu Mengi** (Alama 2 kwa Kila Moja)

Chagua jibu sahihi na uweke herufi ya jibu ulilochagua kwa pengo lililoachwa.

1.________Sheria kuu kabisa katika Biblia inasema:

A. penda jirani yako.
B. penda Mungu.
C. penda marafiki zako.

2.________Mtu akiwa na nia ya uasi kwa Mungu, anahitajika kujitahidi sana kujenga:

A. nia ya heshima.
B. nia ya utumishi.
C. nia ya shukrani.
D. nia ya utulivu.

3.________Nia bora zaidi ya kuwa nayo wakati unatii sheria za Mungu ni kuzitii kwa sababu:

A. unajipenda mwenyewe.
B. wewe ni Mkristo.
C. hutaki kwenda kuzimu.

**Maswali ya Majibu Mafupi**

1. Orodhesha mambo matatu unayoweza kufanya kuonyesha upendo wako kwa Mungu. (Alama 6, kila moja alama 2)

A. ________________________________________
________________________________________

B. ________________________________________
________________________________________

C. ________________________________________
________________________________________

**Maswali ya Majibu Mafupi** *Kuendelezwa*

2. Eleza mambo mawili unayoweza kufanya kuonyesha nia yako ya utulivu kwa Mungu. (Alama 10, kila moja alama 5)

   A. ______________________________

   ______________________________

   B. ______________________________

   ______________________________

3. Orodhesha matokeo matano ya kutii Mungu pamoja na sheria zake. (Alama 2 kwa kila moja)

   A. ______________________________

   B. ______________________________

   C. ______________________________

   D. ______________________________

   E. ______________________________

4. Orodhesha matokeo matano ya kutotii Mungu pamoja na Sheria zake (Alama 2 kwa kila moja)

   A. ______________________________

   B. ______________________________

   C. ______________________________

   D. ______________________________

   E. ______________________________

5. Eleza njia moja ambayo tayari umetendea kazi wiki hii kutokana na kile umejifunza katika kozi hii. Sema vitu halisi ulivyotenda. (Alama 10)

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

6. Andika mistari ya kukariri katika kozi hii. (Alama 12)

# Utiifu kwa Mungu
## Mtihani wa Toleo la 5
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

### Ukurasa wa 1

### Maswali ya Kweli-au Si Kweli
(Alama 2 kwa kila moja)

1. 0 Si kweli
2. X Kweli
3. 0 Si kweli
4. 0 Si kweli
5. X Kweli
6. 0 Si Kweli
7. 0 Si Kweli
8. X Kweli
9. 0 Si Kweli
10. X Kweli
11. 0 Si Kweli
12. 0 Si Kweli
13. X Kweli
14. 0 Si kweli

### Ukurasa wa 2

15. 0 Si Kweli
16. 0 Si kweli
17. 0 Si kweli
18. 0 Si kweli

**Maswali ya Kuchagua Kati ya Majibu Mengi** (Alama 2 kw kila moja)

1. B
2. A
3. B

### Maswali ya Majibu Mafupi

1. Alama 6 (Alama 2 kwa kila moja)
   Majibu yaliyopendekezwa:
   1. Tii sheria za Mungu.
   2. Tii kanuni zilizomo katika sheria za Mungu.
   3. Fanya mapenzi ya Mungu.

# Utiifu kwa Mungu
## Mtihani wa Toleo la 5
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

**Ukurasa wa 3**
**Maswali ya Majibu Mafupi**

2. Alama 10 (Kila moja alama 5)
   Majibu yaliyopendekezwa:

   1. Amini Mungu
   2. Usipingane na viongozi.
   3. Uwe radhi kumtii Mungu. Usitake maelezo kabla ya kumtii Yeye.

3. Alama 10 (Alama 2 kwa kila moja)
   Majibu ya mtu binafsi

4. Alama 10 (Kila moja alama 2)
   Majibu ya mtu binafsi

5. Alama 10
   Majibu ya mtu binafsi

**Ukurasa wa 4**

6. Mistari ya kukariri
   Alama 12, kila andiko alama 6

   Marko 12:30
   Yohana 13:34-35

**Hongera**

________________________________________

Amemaliza

# Utiifu kwa Mungu

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio utaendelea na masomo yako yajayo.

Wakufunzi ___________________________

Tarehe ______________________________

**Hongera**

________________________________________

Amemaliza

Utiifu kwa Mungu

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio utaendelea na masomo yako yajayo.

Wakufunzi ___________________________

Tarehe ______________________________